

HALMASHAURI  
YA WILAYA  
MUFINDI



**VIVUTIO VYA  
UTALII**  
*Karibu ujionee  
na kufurahia  
rasilimali zako*



OFISI KUU, S. L.  
P. 223,  
MAFINGA  
SIMU (026)-  
2772614  
FAX (026)-  
2772070

**Utangulizi:**

Halmashauri ya  
wilaya ya  
Mufindi  
iliundwa

Disemba 31,  
1983 na ilianza  
rasmi shughuli  
zake ikiwa  
halmashauri  
tarehe 1, January  
1984 Wilaya ya  
Mufindi  
inapakana na  
wilaya ya  
Njombe upande  
wa kusini, Iringa  
upande wa  
Kaskazini, Kilolo  
upande wa  
kaskazini  
mashariki, kilom

bero upande wa  
mashariki na  
Mbarali Mbeya  
upande kwa  
upande wa  
Magharibi.

**Vivutio vya utalii  
ndani ya wilaya  
ya mufindi**

Wilaya yetu  
imebarikiwa  
kuwa na vivutio  
mbalimbali  
ingawa bado  
havijatangwazw  
a kwa kiwango  
cha  
kutambuliwa na  
wengi. Baadhi ya  
vivutio hivyo ni:

➤ **Bonde la  
mto  
Kihansi**

Bonde hili  
ndilo  
linalopatikana  
a vyura  
maarufu wa  
Kihansi  
wenye sifa ya  
kuzaa ambao  
hawapatikani  
sehemu  
nyingine  
dunia



**PICHA: Vyura  
adimu wa  
kihansi.**

➤ **Ngome  
ya  
Wajeruma  
ni ya  
Chumumb  
wi**

Ngome hii  
ilijengwa kwa  
lengo la ulinzi na  
mjerumani  
kabla ya vita ya  
kwanza ya dunia  
na ilitumika  
kama kituo cha  
mawasiliano  
ambapo ilikuwa  
na taa zenye  
rangi mbili kijani  
na nyekundu  
ambazo zilikuwa  
zikitumika

kuwasiliana na vituo vingine. Taa ya kijani ilionyesha kuwa hamna hatari na nyekundu iliashiria hatari.



**Picha:Ngome ya Chumumbwi**

➤ **Mapango ya malangali**

Haya ni mapango yenye historia utamaduni wa wahehe

ambapo chifu Mkwawa alikuwa anapumzikia na kupanga mikakati ya kupambana na maadui wakati wa vita. Mapango haya yanatumika kwa ajiri ya matambiko mbalimbali.



**Picha:Mapango ya Malangali**

➤ **Mabwawa ya asili ya Ngwazi na Kihanga**

Haya ni mabwawa matatu makubwa ya asili ndani ya wilaya ambapo kuna shughuli za uvuvi wa kawaida na uvuvi wa burudani pia ni sehemu nzuri ya kupumzika (ufukweni) kupiga picha,kuwekw w kambi(Campi

ng site),kuogele a n.k



**Picha:Boti zinazotumiwa kwa ajili yaSafari fupi za majini ktk bwawa la ngwazi**

Vivutio vingine ni pamoja na Maporomoko ya Galama na Mpanga( Galava and Mpanga water falls),

Msitu wa hifadhi wa Kigogo, Safu ya Milima ya Mufindi(Mufindi plateau), Misisitu ya hifadhi ya Igoda, Ipafu, Lulanda na Msitu wa Asili wa kupandwa wa Millennium, Makorongo ya Mandumbulu, Jiwe la Igangilonga-Igeleke, Kisupo cha Mkwawa (Mkwawa resting place) Sawala, Mashamba ya Chai, haya ni maeneo muhimu na mazuri sana kwa

ajili ya kupiga picha, kuangalia uoto wa asili(Scenic viewing), kufanya tafitimbali pamoja na mambo ya kale.



**Picha:Mianzi pori inayopatikana kwenye msitu wa hifadhi-Lulanda**

**Mapendekezo**

Tunaomba  
Serikali na  
wafanyabiashar  
a wa mambo ya  
utalii  
tushirikiane  
pamoja  
kuwekeza  
kwenye vivutio  
hivi ili jamii na  
Taifa kwa  
ujumla tuweze  
kunufaika na  
rasilimali hizi  
ambazo bado  
hazijapewa  
kipaumbele.

Simu (026)-  
2772663,  
**FAX (026)-  
2772070**

Kijarida hiki  
kimetolewa na  
Idara ya Ardhi,  
Maliasili na  
Mazingira  
S.L.P. 223,  
Mafinga